

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO

Simu: 0262126826
Nukushi: 026 2126834
Baruapepe: km@michezo.go.tz
Tovuti: www.michezo.go.tz



Mji wa Serikali,
Mtumba, Dodoma
2 Mtaa wa Habari,
S. L. P. 25,
40481 DODOMA.

TAARIFA KWA UMMA

**UTEUZI WA BW. ALLY MAYAY KUKAIMU UKURUGENZI WA
MAENDELEO YA MICHEZO**

Septemba 20, 2022 – Dodoma

Katika kuimarisha utendaji kwenye Sekta ya Maendeleo ya Michezo Nchini na kufuatia maelekezo ya Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mhe. Mohamed Mchengerwa, ya kufanya maboresho ili kuongeza tija, Wizara inamtambulisha, Bw. Ally Mayay Tembele kuwa Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Michezo nchini wakati taratibu nyingine zikiendelea.

Bw. Mayay ambaye ni Afisa Mwandamizi katika Mamlaka ya Viwanja vya Ndege nchini, amehamishiwa Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo na kuruhusiwa kukaimu majukumu haya kwa mujibu wa kibali cha Ofisi ya Rais Utumishi kupitia barua yenye kumbukumbu namba CCD.273/311/01/W/45 cha tarehe 15 Septemba 2022.

Uteuzi huo wa Bw. Mayay ambaye anachukua nafasi ya Bw. Yusuph Omary Singo aliyepangiwa majukumu mengine unaanza leo Septemba 20, 2022.

Wadau wa Michezo wanaombwa kumpa ushirikiano katika utekelezaji wa majukumu yake.

Imetolewa na;


John Mapepele

MKUU WA KITENGO CHA MAWASILIANO SERIKALINI